

Majibu ya Vielelezo vya Tathmini (QR5 – Ukurasa wa 220)

Kielelezo cha Kwanza

Gredi ya Saba

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 139-144)

- | | |
|-------|-------|
| 1. C. | 26. A |
| 2. D | 27. C |
| 3. D | 28. C |
| 4. B | 29. A |
| 5. A | 30. B |
| 6. D | 31. C |
| 7. B | 32. B |
| 8. C | 33. B |
| 9. C | 34. A |
| 10. D | 35. B |
| 11. D | 36. B |
| 12. B | 37. B |
| 13. D | 38. A |
| 14. C | 39. D |
| 15. D | 40. B |
| 16. B | 41. A |
| 17. B | 42. C |
| 18. C | 43. D |
| 19. B | 44. C |
| 20. C | 45. C |
| 21. A | 46. A |
| 22. D | 47. C |
| 23. B | 48. D |

24. C 49. A

25. B 50. C

Gredi ya Saba

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 145)

Insha

- Mwanafunzi azingatie muundo wa barua ya kirafiki ambao ni anwani, mtajo, utangulizi, mwili, hitimisho na jina la mwandishi.
- Insha iandikwe kwa kuzingatia sheria za kisarufi.

Utangulizi wa fasihi simulizi

1. a. Fasihi ni kazi inayotumia lugha na ishara kwa ubunifu ili kuwasilisha ujumbe katika jamii.

b.

- kuburudisha wanajamii
- kuelimisha
- kuhifadhi mila na tamaduni za wanajamii
- kuwaleta wanajamii pamoja
- kukashifu matendo maovu katika jamii

c.

- semi
- nyimbo
- hadithi

d.

- Tamthilia
- Novela
- Riwaya
- Hadithi fupi
- Ushairi

Fasihi simulizi

2. a.

- Huu ni wimbo wa watoto.

b.

- Watoto

c.

- Watoto wanapocheza

d.

- Huimbwa kwa kurudiarudia maneno ili kusisitiza ujumbe.
- Huwa na sentensi au kauli fupifupi kwa vile zinaimbwa na watoto, ili waweze kukumbuka kwa haraka.
- Huimbwa na watoto katika michezo yao ya kitoto.
- Huandamana na miondoko ya mwili na muziki.
- Hutungwa kwa ajili ya watoto.
- Huweza kutungwa na watoto wenyewe au mtu mwingine.
- Huweza kuimbwa na watoto wenyewe au watu wengine huku watoto wakisikiliza.
- Huhusu mambo yanayowaathiri na kuwavutia watoto.
- Hutumia lugha nyepesi inayoeleweka na watoto.

e.

- Huwaleta watoto pamoja.
- Huifanya michezo ya watoto kuvutia.
- Huwafurahisha watoto.

f.

- nyimbo za bembelezi
- nyimbo za kazi
- nyimbo za dini

3. Novela

a.

- Huwa na visa na matukio mengi.
- Huwa na wahusika mbalimbali.
- Hutumia lugha ya kisanaa.
- Huwa na ujumbe kwa jamii.
- Huwa ndefu kuliko hadithi fupi.
- Huweza kugawanywa katika sura mbalimbali.

b.

- Mzee Mambo
- Mamake Juma
- Mwanawe mzee Mambo

c.

- Mzee Mambo - mwenye huzuni. Anahuzunika anapomkumbuka mwanawe.
- Mamake Juma - mpenda haki na mlezi mwema, kwani anataka mwanawe abadilike
- Mwanawe mzee Mambo - mchangamfu na mwenye bidii kama anavyomkumbuka babake Mzee Mambo

d.

- Elimu - Kuna suala la elimu katika Shule ya wavulana ya Gwiji. Wanafunzi wanakwenda pale ili wapate elimu.
- Haki - Kesi inaamuliwa na baadaye wanafunzi waliotenda unyama kuhukumiwa kifungo gerezani.
- Mauti - kundi la wanafuzi linateketeza bweni na kusababisha vifo vya wanafunzi wenzao
- Ukatili - Wanafunzi wanaasi sheria za shule na kuwateketeza wenzao katika bweni.

e.

- Mandhari ya mahali - shule ya wavulana ya Gwiji

f.

- Methali - damu ni nzito kuliko maji.
- Msemo - alijikaza kisabuni.

Kielelezo cha Pili

Gredi ya Saba

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 146-151)

1. B
2. C
3. A
4. D
5. B
6. B
7. A
8. B
9. A
10. C
11. B
12. B
13. A
14. B
15. A
16. A
17. B
18. B
19. A
20. B
21. C

22. A

23. B

24. C

25. A

26. B

27. A

28. C

29. B

30. C

31. B

32. B

33. A

34. B

35. B

36. C

37. B

38. D

39. D

40. A

41. A

42. A

43. A

44. A

45. C

46. B

47. B

48. D

49. C

50. A

Gredi ya Saba

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 152-153)

Insha

1. Matumizi ya vifaa vya kidijitali ni kama vile:

- Kutuma na kupokea ujumbe.
- Usambazaji wa habari.
- Matangazo ya biashara.
- Ufundishaji na ujifunzaji.

Umuhimu

- Huwezesha upokeaji na usambazaji wa taarifa.
- Kuunganisha watu kupitia mitandao ya kijamii.
- Huwezesha utafiti wa kielimu na ujifunzaji.
- Hurahisisha biashara kwa kusaidia kufanya matangazo.

Fasihi simulizi

2. (a)

- Huhifadhiwa akilini.
- Husambazwa kwa njia ya mdomo.
- Huwa na fanani.
- Huwa na wahusika mbalimbali.
- Huweza kusahaulika haraka kwa vile huhifadhiwa akilini.

(b) (i) semi (ii) hadithi (iii) maigizo (iv) nyimbo (v) mazungumzo

3. (a) bembelezi

(b)

- Huimbwa na mlezi wa mtoto.
- Huimbwa kwa sauti nyororo.
- Huwa na urudiaji wa maneno.
- Huwa fupi.
- Huambatana na vitendo kama vile kumpapasa mtoto.
- Huwa na ahadi kwa mtoto.

(c) Mamake mtoto – lala mamako nipumzike

(d)

- Husaidia kuongoa mtoto alale au anyamaze.
- Humpa mtoto funzo.
- Hutakasa hisia za mlezi.
- Huburudisha mtoto.

(e) Uradidi – neno kipenzi limerudiwa

Taswira – baba yu njiani

Kisengerembe – atakupa pipi

Novela

4. (a) Huwa na ploti sahili, huwa na usimulizi wa moja kwa moja, huwa na wahusika wachache

(b) jijini Nakuru, mkahawa wa Kitamu

(c) Felista, mwalimu Kristina, Victor na Valeria

(d) mwenye tahadhari, mwenye busara, karimu, aliyewajibika

(e) Mabadiiko – Felista tangu ajiunge na Gredi ya Saba, alikuwa amebadilika sana.

Kuwajibika – Felista aliwalinda wanuna wake kama mboni ya jicho lake.

Elimu - Felista aliwalinda wanuna wake kama mboni ya jicho lake hasa walipoenda na kutoka shuleni.

(f) (i) tashihisi/uhaishaji/chuku

(ii) tashbihi

Kielelezo cha Tatu

Gredi ya Saba

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 154-159)

1.	C
2.	C
3.	A
4.	B
5.	B
6.	B
7.	C
8.	B
9.	C
10.	C
11.	C
12.	C
13.	B
14.	B
15.	C
16.	B

17.	C
-----	---

18. A

19. C

20. D

21.	B
22.	C
23.	D
24.	A
25.	A
26.	A
27.	A
28.	A
29.	C
30.	B
31.	B
32.	B
33.	C
34.	B
35.	A

36.	A
37.	B
38.	B
39.	D
40.	C
41.	C
42.	C
43.	B
44.	A
45.	A
46.	C
47.	A
48.	B
49.	C
50.	B

Gredi ya Saba

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 160-162)

Insha

Zifuatazo ni sehemu kuu zinazopaswa kuzingatiwa katika barua ya kuomba msamaha:

1. Muundo wa barua rasmi

- Anwani ya mtumaji: Ikae upande wa kulia juu (ijumuishe jina la shule na tarehe).
- Anwani ya mpokeaji: Ikae upande wa kushoto, chini kidogo ya anwani ya mtumaji (Mwalimu Mkuu).
- Mtajo
- Mwili wa barua: Mwanafunzi ataje sababu za kuchelewa: k.m. ugonjwa, matatizo ya usafiri, changamoto za kifedha, au dharura ya kifamilia; aonyeshe majuto na kuahidi kutorudia.
- Mwisho wa barua: Hitimisho rasmi (k.m. *Wako mwaminifu*, Sahihi na Jina la mwanafunzi).
- Kichwa cha barua: Kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Kieleze madhumuni (k.m. YAH: OMBI LA MSAMAHA KWA KUCHELEWA KURIPOTI SHULENI).

Fasihi simulizi

2. (a) Fasihi ni sanaa ya kutumia lugha kwa ustadi ili kuwasilisha mawazo, hisia, na ujumbe mbalimbali kwa jamii.

(b) Utanzu ni mgawanyiko au aina kuu za kazi za kifasihi kulingana na sifa na mbinu zake za uwasilishaji. Mfano wa utanzu ni hadithi, methali, vitendawili, nyimbo, ngano, riwaya, tamthilia, mashairi.

(c) Fasihi simulizi.

(ii) Fasihi andishi.

(d)

- Hutegemea matumizi ya mdomo/kumbukumbu: Huonekana wazee wanaposimulia ngano jioni.
- Hubadilika kulingana na hadhira/mazingira: Msimulizi huongeza au kupunguza maneno kulingana na umri wa wasikilizaji.
- Hushirikisha hadhira moja kwa moja: Hadhira huitikia (k.m. *Paukwa - Pakawa*) au kuimba pamoja na msimulizi.
- Huwasilisha mafunzo kupitia burudani: Watoto hufundishwa maadili kupitia nyimbo na vitendawili.

(e) Fasihi Simulizi: Ni bora kwa sababu huwasilishwa kwa mdomo na kushirikisha jamii nzima papo hapo, hivyo kurithishwa kwa vizazi kwa urahisi bila kuhitaji ujuzi wa kusoma.

Fasihi Andishi: Ni bora kwa sababu haibadiliki kirahisi kwani inapoandikwa hudumu kwa muda mrefu sana kwenye vitabu au mitandao bila kusahaulika.

3. (a)

Bembelezi: Ni wimbo unaoimbwa na mzazi au mlezi ili kumtuliza au kumfanya mtoto alale.

(b) Mzazi (Mama au Baba)

Mtoto/Malaika

(c)

- Takriri/Urudiaji: Kurudia maneno kama "Lala lala".
- Tashihisi: "Pepo wanapuliza" au "Nyota zakulinda"
- Istiara: Kumwita mtoto "malaika wangu".

(d)

- Humpa mtoto utulivu wa kisaikolojia na kumwondolea woga ("Usiogope niko hapa").
- Hujenga uhusiano wa karibu na upendo kati ya mzazi na mtoto.
- Husaidia mtoto kupata usingizi mzuri na wa amani.

(e)

- Kutumia ishara za mikono na mwili (k.m. kuiga kubembeleza mtoto au kufumba macho).
- Kubadilisha kiwango cha sauti (kuimba kwa sauti ya chini, laini na ya kutoa utulivu).
- Kuhusisha darasa (kuhimiza wenzako kuitikia au kuimba kiitikio).

Novela

4. (a)

- Ina msuko sahili/ mwepesi unaofuatika kwa urahisi (safari ya Andere).
- Idadi ndogo ya wahusika (Andere, Mama na Baba pekee).
- Inajikita kwenye tukio moja kuu (uamuzi wa Andere kuondoka kijijini kwenda Nairobi kufuata ndoto yake).
- Mandhari yake ni finyu/ machache (kando ya barabara, nyumbani kwao).
- Ni fupi.

(b) Dhamira kuu ni kupambana na umaskini/ kufuata ndoto/ umuhimu wa malezi na ushauri wa wazazi.

(c) Andere, Mama yake, au Baba yake.

(d)

- Tashihisi: "Jua lilikuwa linazama polepole...", "moyo wake ulidunda...", au "mabati yaliyopiga kelele..."
- Istiara: "Ndoto yake haikuwa tena kivuli..."
- Msemo: "kupiga kelele", "kuona mwanga mbele".

(e)

- Mandhari ya mahali - barabarani : Pale Andere aliposimama akitazama basi likitoweka; nyumbani/ kijijini/ ndani ya nyumba ndogo - ambapo mazungumzo kati ya Andere na wazazi wake yalifanyika.
- Mandhari ya hali – Wasiwasi na upendo
- Mandhari ya wakati – Usiku ulipoingia

Kielelezo cha Nne

Gredi ya Nane

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 163-167)

1. B
2. C
3. C
4. B
5. C
6. B
7. B
8. C
9. B
10. B

11. C

12. B

13. B

14. B

15. C

16. C

17. B

18. B

19. B

20. B

21. B

22. C

23. C

24. B

25. B

26. A

27. B

28. B

29. A

30. A

31. C

32. B

33. A

34. B

35. B

36. D

37. A

38. C

39. B

40. A

41. B

42. A

43. C

44. C

45. B

46. B

47. B

48. A

49. B

50. B

Gredi ya Nane

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 168-170)

Insha

1.

- Insha iwe na maneno kati ya 300-350.
- Kisa kiwe cha kulisimua na chenye lugha ya mvuto.
- Makosa ya sarufi na hijai yaepukwe.
- Kisa kihusiane na jambo baya ambalo lilitokea shuleni ambalo lilimfanya kila mwanafunzi awe na hofu.

Fasihi simulizi

2 (a). Wahusika ni wanyama kama vile: Sungura, Simba, Tembo na Swala ambao wamepewa tabia za binadamu kama vile kuzungumza na kufanya kazi (kuchimba kisima) kama binadamu.

(b).

- Sungura ni mjanja- alijifanya kuwa ni mgonjwa hivyo akakataa kushiriki katika kuchimba kisima.
- Kasa ni mwajibikaji- alilinda kisima usiku kucha.
- Tembo na Swala ni wenye bidii- walijitolea kwa hali na mali katika kuchimba kisima
- Simba ni kiongozi bora kwani alitafuta mbinu ya kupata maji kijijini.

(c).

- Umoja na ushirikiano - wanyama walishirikiana katika kuchimba kisima ambacho kiliwasaidia kupata maji.
- Ujanja una mwisho, Sungura alitumia ujanja kuteka maji kutoka kwa kisima ambacho hakuchimba na mwisho wake akanaswa.
- Uvivu una hasara zake kwani kutokana na uvivu wa sungura alinyimwa nafasi ya kuteka maji.

(d).

- Methali: Ujanja wa nyani huishia jofuni
- Nidaa: hauruhusiwi kunywa maji hapa!
- Taswira: kisima kilikuwa kimechafuliwa kwa matope.

(e). Mtu anayedhani kuwa ni mjanja mwishowe ujanja wake hufika kikomo na kunaswa.

Novela

3 (a).

- Umaskini: Juma walikuwa wanaishi kwenye mtaa wa mabanda, alikuwa akisomea kwenye mwanga wa vibatari.
- Elimu: elimu ni ufunguo wa kutoa watu katika lindi la umaskini.
- Bidii: Mama Juma alitia bidii katika kumwelimisha Juma ili kumhakikishia maisha mazuri ya usoni.

(b).

- Mtaa wa mabanda: mandhari haya yanamfanya Juma kusomea mwanga wa vibatari.
- Watu wanaoishi katika mandhari haya ni wa tabaka la chini kwa hivyo mandhari haya yanampa Juma motisha ya kutia bidii masomoni ili afanikiwe na kutoka kwenye lindi la umaskini.

(c).

- Juma anapokea matokeo ya mtihamu kwa furaha na kuibuka mwanafunzi bora.
- Kumbukumbu ya changamoto zake kama kusoma kwa kibitari na umaskini.
- Mazungumzo ya faraja na mamake ya kumkumbusha kutia bidii.
- Juma kuapa kupambana ili kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari.

(d).

- Mwenye bidii: alitia bidii katika kumwelimisha Juma ingawa alikuwa mgonjwa.
- Mshauri mwema: anamwambia Juma kuwa masomo yake ndiyo ufunguo wa kuwatoa katika lindi la umaskini.
- Mwenye matumaini: alikuwa na matumaini kuwa maisha ya usoni yatakuwa mazuri kwa sababu ya bidii ya Juma masomoni.
- Mlezi mwema: ingawa alikuwa maskini alijaribu juu chini ili kumwelimisha Juma.

(e). Istiari: amelinganisha umaskini na lindi (shimo kubwa).

Tamthilia

4 (a).

- Ni ya kutoa maaagizo ya jukwaani hasa kwa wale wanaoigiza.
- Humsaidia msomaji kuelewa mandhari kwa kina.
- Humsaidia kujua matendo na hisia za waigizaji.

(b).

- Kuhimiza usawa wa kijinsia katika elimu kwani mtoto wa kike na wa kiume wana nafasi sawa.
- Kupinga mila na tamaduni zilizopitwa na wakati.

(c).

- Mgogoro kati ya Baba na mtoto- kuna mgogoro kati ya Mzee Tembo na Linet kwa sababu mzee Tembo amemlipia ndugu yake karo akamwacha Linet kwa kuwa ni msichana
- Mgogoro kati ya ukale na usasa. Tamduni zilikuwa zinamkandamiza mtoto wa kike nafasi ya elimu ilhali usasa unathamini elimu ya kila mtoto na pia usasa unasisitiza usawa katika jinsia mbili.

(d).

- Ni jasiri: Anamwambia baba yake uso kwa uso kuwa hawezi kuvumilia kufukuzwa shuleni ilhali kaka yake anaendelea kusoma.
- Amepevuka kiakili: anamfahamisha baba yake kuwa elimu ni haki ya kila mtoto.
- Ana msimamo thabiti: anamwambia baba yake kuwa hawezi kukubali ndoto zake zizikwe hai.

(e).

- Mdokezo: “na utamaduni wetu unasisitiza...”
- Nidaa: “Katiba ya sasa inalinda haki zangu!”
- Tashihisi: sitakubali ndoto zangu zizikwe hai
- Taswira: tumechorewa taswira ya sebule ya Mzee Tembo.

Ushairi

5.(a) Lina beti tano

Kibwagizo: Heshima kwa tamaduni, ni wajibu wetu sote.

(b). Ubeti huu unaeleza kuwa hatupaswi kucheka lugha au mavazi wawaayo watu kwa sababu kila mtu ana asili yake. Hivyo ni vyema tuheshimu tamaduni za kila mtu.

(c).

- Amani itatawala.
- Chuki na ubaguzi utaisha
- Dunia itakuwa kama paradiso ambapo hakutakuwa na njaa.

(d). Dunia itakuwa paradiso

Tamaduni za dunia ni pambo la mwanadamu

(e). Mwanadamu, mtu

Kielelezo cha Tano

Gredi ya Nane

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 171-175)

1	B	11	B	21	B	31	A	41	D
---	---	----	---	----	---	----	---	----	---

2	B	12	C	22	C	32	A	42	B
3	D	13	C	23	C	33	C	43	A
4	A	14	C	24	C	34	D	44	D
5	C	15	D	25	C	35	B	45	C
6	D	16	A	26	B	36	C	46	B
7	B	17	B	27	A	37	C	47	D
8	C	18	C	28	D	38	B	48	D
9	A	19	C	29	C	39	B	49	A
10	D	20	C	30	A	40	C	50	D

Gredi ya Nane

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 176-178)

Insha

1. Baadhi ya hoja ni:

- Kutambua na kukubali hisia zako.
- Kutumia mbinu za kutuliza mwili na akili.
- Kubadilisha namna unavyofikiri.
- Kuchukua muda kabla ya kufanya maamuzi.
- Kutafuta msaada kutoka kwa mtaalamu.

Fasihi simulizi

2. (a) hekaya (b) mighani (c) visasili

3. (a) (i) hurafa

(ii) Ina wahusika wanyama ambao ni Punda na Pundamilia

(b) Punda na Pundamilia

(c)

- Mwenye tamaa – alingoja kwa tamaa afanane na nduguye Pundamilia.
- Hajawajibika – alirukaruka na kumwaga rangi.

(d) Tusiwabague wenzetu – Pundamilia alikataa katakata kuandamana na Punda kwenye sherehe.

(e) (i) msemu (ii) tashbihi

Novela

4. (a) barabarani, ofisini mwa Mwalimu Mkuu

(b) Haki ya kupata elimu, haki ya kufanya maamuzi na haki ya kutangamana

(c)

- Mpole – alitamka kwa upole
- Amewajibika – anamweleza Bwana Kato kuwa Toti ana haki mbalimbali
- Mtetezi wa haki – anamweleza Bwana Kato kuhusu haki za Toti

(d) Toti anaenda shuleni. Bwana Kato anamfuata shuleni kwa hasira. Anajipata ofisini mwa Mwalimu Mkuu. Mwalimu Mkuu anamweleza kuwa Toti ana haki ya kupata elimu. Bwana Kato anapositiza kuwa hataki Toti awe shuleni, Mwalimu Mkuu anasema kuwa sheria itachukua mkondo wake. Inabidi Bwana Kato anyenyekee.

(e) (i) tanakali ya sauti

(ii) methali

Tamthilia

5. (a) sebuleni

(b)

- Ina maelekezo ya jukwaani.
- Huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo.

(c)

- Uwajibikaji – mama anajaribu kumpa Ali dawa ili apone.
- Kutowajibika – Mama anajaribu kumpa Ali dawa bila ushauri wa daktari.

(d)

- Mwenye msimamo thabiti – anakataa katu kunywa dawa anazopewa kwa vile hajamwona daktari.
- Mwenye kumbukumbu nzuri – anakumbuka alichambiwa na mwalimu wake kuhusu matumizi ya dawa.

- Amemakinika – anaweza kugundua kuwa dawa anazopewa zimekaa chini yam to kwa zaidi ya mwaka mmoja.

(e)

- Tashbihi – kichwa kinaniwanga kama ngoma ya wanga
- Kisengerenyuma – zilimponya dadako alipokuwa na homa kama yako mwezi uliopita
- Nidaa – La mama!
- Utohozi – hospitalini
- Taswira – anakuja mbio kutoka jikoni

Kielelezo cha Sita

Gredi ya nane

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 179-183)

1. A	11. C	21. B	31. A	41. C
2. C	12. A	22. C	32. A	42. C
3. D	13. A	23. A	33. B	43. A
4. C	14. D	24. C	34. A	44. A
5. C	15. A	25. B	35. C	45. B
6. C	16. C	26. A	36. B	46. B
7. C	17. B	27. B	37. D	47. C
8. D	18. B	28. C	38. D	48. C
9. C	19. A	29. A	39. A	49. C
10. B	20. A	30. B	40. B	50. C

Gredi ya Nane

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 184-186)

Insha

ZOEZI I: HOTUBA KUHUSU UMUHIMU WA NIDHAMU SHULENI

Insha hii iandikwe kwa kuzingatia mambo yafuatayo: **Muundo, Maudhui, na Lugha.**

a. Muundo wa Hotuba

- **Kichwa:** Kionyeshe msemaji, hadhira, mada, mahali na tarehe (Kwa mfano: *Hotuba ya kiongozi wa wanafunzi kuhusu umuhimu wa nidhamu shuleni*).
- **Utangulizi/Itifaki:** Kuanza kwa kuamkua hadhira kwa kuzingatia vyeo na hadhi. (Kwa mfano: *Mwalimu Mkuu, walimu na wanafunzi wenzangu, hamjambo...*).
- **Mwili:** Ufafanuzi wa mada kwa aya mbalimbali ukihusisha hadhira. (Kwa mfano: *Ndugu wanafunzi..., Kama mnavyojua...*).
- **Hitimisho:** Kushukuru hadhira kwa kukusikiliza. (Kwa mfano: *Asanteni kwa kunisikiliza.*).

b. Maudhui

Mwanafunzi afafanue umuhimu wa nidhamu shuleni. Hoja zinaweza kuwa:

- Inasaidia katika kuboresha matokeo ya kimasomo na kitaaluma.
- Inajenga uhusiano mwema kati ya wanafunzi na walimu/wafanyakazi wa shule.
- Inalinda na kuhifadhi mali ya shule na kuzuia uharibifu.
- Inasaidia kupunguza visa vya adhabu na kufukuzwa shuleni.
- Inajenga msingi wa tabia njema na uongozi katika mustakabali wa maisha ya baadaye.

c. Lugha

- **Matumizi ya lugha:** Lugha ya kutoa ufafanuzi, yenye adabu na ushawishi.
- **Msamiati:** Matumizi ya msamiati mwafaka wa mazingira ya shule na maadili.
- **Sarufi:** Kuzingatia muundo wa sentensi, uakifishaji sahihi na tahajia bila makosa.
- **Urefu:** Maneno kati ya 300–350.

Fasihi simulizi

2. (a)

- Mighani

(b)

- Ujasiri wa kweli hauji kwa nguvu za kimwili pekee, bali kwa kuwa na moyo mwema, hekima na uwezo wa kusaidia wenye shida.

- Umoja na ushirikiano ni nguzo muhimu katika kulinda na kuendeleza jamii.

(c)

- Uwindaji
- Uvuvi
- Biashara

(d)

- **Mwenye ujasiri/shupavu:** Hakuogopa kwenda kupambana na Joka la Moto ambalo kijiji kizima kililiogopa.
- **Mwenye huruma/mkarimu:** Alimpa mwanamke mzee chakula chake kidogo alipokuwa njiani.
- **Mwenye hekima/mjanja:** Alitumia mbinu ya kelele na kupiga ngao badala ya nguvu pekee kumshinda joka.
- **Mnyenyekevu:** Aliporudi kijijini, hakujiwunia ushindi wake pekee bali alihimiza watu washirikiane.

(e)

- **Mandhari ya mahali:** Milima ya Ukalo, kijiji, pango la joka.
- **Mandhari ya hali:** Hofu kuu (wakati joka lilipovamia), hali ya utulivu/furaha (baada ya ushindi).
- **Mandhari ya wakati:** Tangu siku hiyo...

(f)

- Matumizi ya ishara za mikono na mwili (miondoko).
- Kubadilisha sauti/kiwango cha sauti kulingana na uhusika.
- Matumizi ya mihemko ya uso kama vile vicheko au sura ya hofu.
- Kushirikisha hadhira kama vile kwa nyimbo au maswali.

(g) Wema hulipwa na wema - Mwandu alimsaidia ajuza akabarikiwa na kupewa siri ya ushindi.

- Nia thabiti na hekima huleta ushindi dhidi ya matatizo makubwa.

Novela

3. (a)

- Inajenga hisia ya hadithi (Kwa mfano: *usiku wa manane* na *baridi* huleta hisia za uzito au siri).
- Yanaibua tabia au hali ya mhusika (Kwa mfano: *anga jeusi kama uso wa hasira* linaonyesha ukali wa siku ya makabiliano).
- Yanasaidia kujenga ploti/matukio ya hadithi.
- Yanatambulisha wahusika.
- Yanaonyesha matendo ya wahusika.

(b)

- **Mandhari ya mahali:** Mji wa Kalevu, vichochoro, chini ya mti mkongwe, shamba.
- **Mandhari ya wakati:** Usiku wa manane, majira ya mvua, mchana wa jua kali.

(c) **Tashbihi:** "...mwezi uking'aa kama taa...", "...Amani... aonekane kama mzee...", "...macho yanayong'aa kama fedha..."

- **Istiar:** Bi. Rehema kuwa "...nguzo ya nyumba..."
- **Nahau:** "...alimeza mate ya moto..." (kuona aibu/shida).
- **Tashihisi:** "...asili yenyewe ilikuwa ikisherehekea...", "...dhuluma ikiota mizizi..."

(d)

- **Jasiri:** Hakubali dhuluma wanayotendewa watu na anawaongoza vijana kupambana na Bw. Kilonzo.
- **Mwenye busara/hekima:** Anatumia ushahidi wa maandishi na ujanja badala ya vita vya nguvu.
- **Mnyenyekevu:** Hajivuni baada ya ushindi; anabaki "kama tunda lililoiva".

(e)

- Amani analelewa na mama yake (Bi. Rehema) kwa maadili na hekima.
- Anashuhudia dhuluma ya ardhi inayofanywa na Bw. Kilonzo kijijini.
- Anawahamasisha na kuwaunganisha vijana wenzake chini ya mti mkongwe ili kupinga dhuluma.
- Siku ya makabiliano, anatumia ujanja na ushahidi wa maandishi kumshinda Bw. Kilonzo na kurudisha ardhi, kisha anabaki kuwa kielelezo cha unyenyekevu.

Tamthilia

4. (a)

- Kuhimiza umuhimu wa subira na bidii ya halali katika kutafuta maisha badala ya kutafuta utajiri wa haraka (njia za mkato).
- Kuonya vijana dhidi ya tamaa inayoweza kuwaponza na kuwaharibia maisha yao na heshima zao.

(b)

- **Kielelezo cha mandhari ya ndani ya hali:** Uhusiano wa "uso wa wasiwasi" wa Tunu unajenga mgogoro wa ndani na kuonyesha shinikizo la kimaisha analopitia kijana huyo kabla ya kurekebisha na wazee.
- Inasaidia kuonyesha mabadiliko ya mhusika (Kwa mfano: Anga linaanza kutulia wakati Tunu naye anapoanza kuelewa na kutulia).
- Kujenga ploti.
- Kuibua wahusika na matendo yao.
- Kuibua tamathali kama vile taswira.

(c)

1. **Mzee Fumbo:**

- *Sifa:* Mwenye busara/hekima - anamshauri Tunu kwa methali; Mwenye subira/mchapakazi – anajishughulisha na ufinyanzi wa vyungu.

2. **Tunu:**

- *Sifa:* Mwenye tamaa - anataka utajiri wa njia ya mkato; Mwenye kukubali ushauri/mwelewa - mwishowe anakubali makosa na kuamua kuanza upya.

3. **Rehema:**

- *Sifa:* Mshauri mwema/mwenye kujali - anamuunga mkono Mzee Fumbo kumsaidia Tunu asipotee.

(d)

- **Tamaa:** Tunu anataka kupata utajiri kwa njia ya mkato kwa sababu ya kuchoshwa na umaskini.
- **Elimu/Ushauri:** Mzee Fumbo na Rehema wanampa Tunu mafunzo na semi za kumwelekeza kwenye maadili.
- **Majuto/Mabadiliko:** Tunu anajuta na kukiri kwamba amekuwa akifanya makosa ("nimekuwa nikikimbiza upepo") na anaamua kubadilika.

Kielelezo cha Saba

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 187-191)

1	C	11	D	21	A	31	B	41	D
2	A	12	B	22	D	32	B	42	B
3	C	13	D	23	D	33	A	43	D
4	D	14	C	24	B	34	B	44	C
5	C	15	C	25	B	35	C	45	D
6	A	16	A	26	B	36	D	46	A
7	C	17	A	27	A	37	C	47	D
8	A	18	A	28	C	38	B	48	B
9	B	19	C	29	B	39	B	49	C
10	D	20	A	30	A	40	A	50	D

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Pili (ukurasa wa 192-194)

Insha

1. Hakikisha umezingatia muundo wa shajara. Kuwe na siku na tarehe kisha matukio ya siku hiyo.

Fasihi simulizi

2. (a) Kuna mtegaji, mteguaji na kuna fumbo ambalo linafumbuliwa.

(b) Mtegaji anatangaza kitendawili kisha mteguaji anasema tega. Kisha kitendawili kinatolewa. Mteguaji anaposhindwa kukijibu, anampa mtegaji mji kisha anapewa jibu.

(c) huburudisha, huleta watu pamoja, hukuza uwezo wa kufikiri, huelimisha

(d) (i) methali (ii) tashbihi (iii) msembo

Novela

3. (a) bonde lililokauka

(b)

- Awali, bonde hilo lilikuwa kijani ila sasa lilikuwa limegeuka kuwa kama jangwa la Kalahari
- Awali, swara, tumbili na ndege walikuwa wengi ila sasa hawakuwepo.
- Miti ilikuwa mingi awali ila sasa kulikuwa na visiki tu.
- Mto uliojaa maji sasa ulikuwa tu mtaro usio na maji.
- Mzee Babu alipokuwa kijana walikuwa wakikata mti mmoja wanapanda miwili lakini sasa watu walikata miti bila kupanda mingine.

(c)

- Mwenye kumbukumbu nzuri – anakumbuka jinsi eneo hilo lilivyokuwa kijani ujanani mwake.
- Amewajibika – Anahuzunika kuona jinsi ambavyo konde limekauka sasa.

(d)

- Kuonyesha madhara ya kutowajibika kutunza mazingira.
- Kuwahamasisha watu kutunza mazingira.
- Kuonyesha nafasi ya vijana katika kutunza mazingira.

(e)

- Taswira – Mzee Babu alisimama huku kajitwika mikono kichwani.
- Uhaishaji – macho yake yaliyochoka
- Msemo – tayari amekula chumvi nyingi

Tamthilia

4. (a) Kuonyesha kuwa usalama barabarani unafaa kupewa kipaumbele kila wakati.

(b) barabarani, kwenye stendi ya pikipiki

(c) Uwajibikaji – Amani anataka Kambo awajibikie usalama wa abiria kwa kuwapa helmeti.

Kutowajibika – Kambo anaendesha pikipiki bila kuvaa helmeti.

(d)

- Amewajibika – Amani anajali usalama wake kwa kuomba apewe helmeti.
- Mwenye msimamo thabiti – anakataa katu kupanda pikipiki ya Kambo kwa vile hajapewa helmeti.

(e)

- Istiara – sisi ndio wafalme wa kasi
- Kisengerembele – kesho nitakuwa nimenunua
- Taswira – anaivaa helmeti
- Nahau – inang’oa nanga

Ushairi

5. (a) Mwananchi anayehimiza wazingatie na kulinda maadili.

(b) umoja, uzalendo, uadilifu, heshima

(c)

- Shairi hili lina beti tano.
- Kila ubeti una mishroro minne.
- Kila mshororo una vipande viwili.
- Kila mshororo una mizani kumi na sita.
- Shairi lina kibwagizo ambacho ni, ‘Ma’dili tuzingatiye, na tuweze kuyalinda’.
- Vina vinatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

Kielelezo cha Nane

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 195-200)

1. B
2. C
3. A
4. C

5. C

6. B

7. B

8. B

9. C

10. C

11. A

12. A

13. B

14. C

15. B

16. A

17. C

18. D

19. C

20. B

21. A

22. A

23. A

24. B

25. A

26. B

27. B

28. C

29. B

30. B

31. B

- 32. C
- 33. A
- 34. B
- 35. B
- 36. A
- 37. C
- 38. B
- 39. A
- 40. C
- 41. B
- 42. B
- 43. A
- 44. A
- 45. B
- 46. B
- 47. B
- 48. B
- 49. C
- 50. C

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Pili (ukurasa 201-202)

Insha

- (a) Insha iwe na maneno kati ya 300-350.
- (b) Kisa kiwe cha kuisimua na chenye lugha ya mvuto.
- (c) Makosa ya sarufi na hijai yaepukwe.
- (d) Kisa kihusiane ajali ya barabarani au jambo ambalo ulishuhudia barabarani.

Fasihi simulizi

2. (a) Wimbo wa kazi: Mtunzi anasema kuwa maghala yao yapate kujaa nafaka tele.

(b).

- Kuwahimiza watu kutia bidii na kukashifu uvivu.
- Hutumiwa kama burudani na kuondoa uchovu kwa wanaofanya kazi.
- Kuhimiza ushirikiano katika kazi.

(c).

- Tashihisi: Jembe langu thabiti, pasua ardhi hii ngumu
- Chuku: pasua ardhi hii ngumu.

(d).

- Kutia bidii kazini
- Kufanya kazi kwa umoja na ushirikiano.
- Kupinga au kukashifu uvivu.

(e). Mafanikio au mazao yanayopatikana baada ya kufanya kazi fulani.

Novela

3 (a). Biashara yake ya matunda na mboga imepata soko jipya na wateja wamekuwa wengi hata kutoka kwa vijiji jirani.

(b). Alifikiri kuwa teknolojia ilikuwa ya watu wa mjini tu.

(c).

- Wingi wa oda/ bidhaa ambazo wateja walihitaji.
- Uhaba wa usafiri wa pikipiki.

(d).

- Kufikia soko mpya na kubwa kwa urahisi kupitia kwa kutangaza bidhaa zao.
- Kuwasiliana na wateja kwa urahisi.

(e).

- Barabara
- Pikipiki

Tamthilia

4. (a). Tumaini anataka miti iliyo kando ya chemchemi ya maji ikatwe kwa sababu watapewa mamilioni ya pesa ila Mzee Mzalendo anakataa kwa sababu anathamini utunzaji wa maliasili.

(b). Anaamini kuwa ni jukumu lao la kibinafsi la kutunza mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo na hivyo basi anakataa kutia sahihi yoyote itakayochangia katika kuharibu urithi wao.

(c).

- Jamii itakabiliwa na ukame
- Magonjwa yatawashambulia
- Kijiji kitakosa maji safi

(d).

- Mwajibikaji - anafahamu kuwa jukumu la kutunza mazingira ni lake.
- Mpevu - anasema kuwa mamilioni ya pesa ambazo watapewa ni kama moshi, haziwezi kulinganishwa na mazingira.
- Mzalendo - anatetea haki za binadamu kupitia kwa utunzaji wa mazingira.

(e). *Akihema*: Inadhihirisha kuwa ni mwepesi wa kushawishika na ndio sababu alimwendea baba yake akihema.

Kwa sauti ya kulalamika: hakuridhishwa na mtazamo wa baba yake wa kutunza mazingira.

Ushairi

5 (a). Mshikamano wa jamii/mshikamano wa dhati/umoja ni nguvu

(b). Mshikamano wa dhati, ndio nguzo ya amani.

(c). Maadili (ya kitaifa).

(d). Beti tano

(e).

- Kutombeza au kutomfanyia mwenzako kebehi anapopata shida.
- Kukimbia kumsaidia jirani/ mwenzako kwa ari na upendo anapokuwa na shida.

Kielelezo cha Tisa

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 203-207)

1. A	11.C	21.C	31.C	41.C
2. D	12.B	22.A	32.D	42.D
3. A	13.D	23.A	33.A	43.C
4. C	14.A	24.C	34.B	44.A
5. A	15.D	25.B	35.D	45.B
6. B	16.A	26.A	36.C	46.D
7. B	17.A	27.B	37.B	47.D
8. B	18.B	28.A	38.D	48.D
9. C	19.C	29.B	39.B	49.B
10. C	20.C	30.A	40.C	50.B

Gredi ya Tisa**Karatasi ya Pili (ukurasa wa 208-210)**

1 (a). Kisa kioane na maana ya methali uliyopewa.

(b) Insha iwe na maneno kati ya 300-350.

(c) Epuka makosa ya hijai.

Fasihi simulizi

2.

(a) hurafa- wahuika wake ni wanyama.

(b) –

- Wahuika wake ni wanyama
- Wanyama wamepewa sifa za binadamu. Kwa mfano: Kobe ana deni la Chui

(c)

- Methali- Mbio za sakafuni huishia ukingoni.
- Nahau- Pata afueni
- Swali la balagha - Nitamwambiaje kuwa nilimsaliti?

(d) Chui, Kobe, Sungura

(e) Kobe alikataa kulipa deni la Chui.

(f)

- Msaliti-anamsaliti rafikiye Kobe kwa kumwonyesha Chui walikofichwa watoto wa Kobe.
- Mwenye majuto - anajutia kitendo chake cha usaliti.

Novela

3.

(a)

- Urefu wa kadri
- Maudhui machache
- Wahusika wachache
- Ploti sahili
- Mandhari finyu
- Fani chache za lugha.

(b)

- Mandhari ya mahali-Gereza Kuu la Badilika
- Mandhari ya wakati- saa za asubuhi

(c)

- Vita - Mui na wenzake wanafungwa gereza kwa kusababisha vita vya kikabila.
- Uharibifu - Mui na wenzake wanateketeza mali ya watu wa kabila tofauti na lao.
- Kifo - wenzake Mui waliokuwa wamefungwa gereza waliaga dunia.
- Elimu - akiwa gereza, Mui anaendelea na masomo yake.
- Mabadiliko - Mui anabadilika akiwa gereza na kuwa mhubiri mashuhuri na mchamungu. Anajirudi na kujutia matendo yake.

(e)

- Tashbihi - fuata upepo kama bendera.

- Methali - maji yakimwagika hayazoleki, asiye funzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
- Nahau - gonga mwamba
- Maswali ya balagha - Watamkubali katika ulimwengu huru?

(f)

- Mwenye majuto - anajuta kitendi kilichompeleka gereza ni na hata kuandika barua za kuomba msamaha kwa wanakijiji
- Ni mchamungu - ana uzoefu wa kusali na pia ni mhubiri.

Tamthilia

4.

(a)

- Elimu- Yusufu anatoka shuleni.
- Migomo- wanafunzi wanafanya migomo wakiwa shuleni na kurudi nyumbani.
- Mawaidha- wazazi wake Yusufu wanampa mawaidha; aepukane na vurugu shuleni.

(b)

- kujua mandhari.
- kujua hisia na matendo ya wahusika.
- kujua sifa za wahusika.

(c)

- Matendo ya wahusika yamewekwa katika mabano.
- Majina ya wahusika yamewekwa katika upande wa kushoto na maneno yao katika upande wa kulia.
- Imegawika katika sehemu na maonyesho.

(d)

- Mandhari ya mahali-nyumbani kwa Mzee Majuto

- Mandhari ya wakati- saa mbili asubuhi.

(e)

- Uzungumzi nafsi- Mzee Majuto anajizungumzia
- Uradidi-neno mgomo na migomo limerudiwarudiwa
- Methali- mvumilivu hula mbivu
- Nahau- kata kauli
- Tashbihi- wakaidi kama mkia wa mbuzi

Ushairi

5.

(a)

- Shairi lina lina beti tatu.
- Kila ubeti una mishororo minne.
- Kila ubeti umegawika katika vipande viwili, utao na ukwapi.
- Shairi hili lina kibwagizo.

(b) Nafsineni ni mama anayempa mwanawe wosia au mawaidha.

(c) Methali- heshima si utumwa

(d)

- Mawaidha/wosia. Nafsinenewa anapewa ushauri awe na heshima na asiandamane na watu wabaya.
- Elimu- anaambiwa anapokuwa shuleni aepukane na marafiki wabaya.

Kielelezo cha Kumi

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Kwanza (ukurasa wa 211-216)

1. C

2. C

3. C

4. B
5. C
6. C
7. A
8. C
9. D
10. A
11. B
12. D
13. C
14. B
15. C
16. C
17. B
18. C
19. C
20. D
21. B
22. C
23. B
24. C
25. D
26. B
27. A
28. C
29. A
30. D

31. B

32. D

33. A

34. A

35. B

36. C

37. C

38. A

39. D

40. D

41. A

42. B

43. B

44. B

45. A

46. C

47. C

48. A

49. B

50. B

Gredi ya Tisa

Karatasi ya Pili (ukurasa wa217-220)

Insha

1. Barua rasmi ya kuomba msaada wa karo

(a) Zingatia muundo wa barua rasmi.

- Anwani ya mtumaji: Ikae upande wa juu kulia.

- Tarehe: Iandikwe chini ya anwani ya mtumaji.
- Anwani ya mpokeaji: Ikae upande wa kushoto, chini kidogo ya tarehe.
- Mtajo: Salamu ya kufungua kama vile *Kwa Bwana/Bibi*, au *Mpendwa Mfadhili*.
- Kichwa cha barua: Kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Kionyeshe dhumuni: Kwa mfano: **YAH: MAOMBI YA MSAADA WA KARO YA SHULE.**
- Mwili wa barua: Utangulizi, maelezo ya kina na hitimisho.
- Salamu ya kufunga: Kama vile *Wako mwaminifu*, ikifuatiwa na saini na jina la mtumaji.

(b) Zingatia maudhui ya barua yako.

(c) Tumia lugha rasmi na sahihi.

(d) Zingatia toni ya unyenyekevu.

(e) Hakikisha insha yako ina maneno 300–350.

Fasihi simulizi

2.

(a) Hekaya - Hadithi za wanyama ambapo wahusika hupewa sifa za kibinadamu ili kutoa maadili na mafunzo katika jamii.

(b)

- Kilimo - kulima nafaka na mboga na kupanda mbegu).
- Biashara - kubadilishana mazao na kuanzisha soko la kila wiki.
- Uongozi/Mikutano ya kijamii.

(c)

- Mwenye hekema/busara: Anawaongoza wanyama na kuwakumbusha umuhimu wa umoja wakati wa ukame.
- Kiongozi bora: Anasimamia mikutano na maendeleo ya kijiji.

(d)

- Mandhari ya mahali: msitu wa Amani, Kijijini, chini ya mti wa mbuyu, sokoni.
- Mandhari ya wakati: Kila wiki
- Mandhari ya hali: Upendo, ushirikiano na umoja.

(e)

- Matumizi ya mabadiliko ya sauti/ toni: Kuiga sauti za wanyama tofauti kama vile simba au ndovu.
- Lugha ya ishara: Kutumia mikono, macho na uso kuonyesha matukio kama vile ukame au furaha ya harusi.
- Kushirikisha hadhira: Kupitia maswali ya balagha au nyimbo za sherehe jukwaani. (

(f)

- Kiongozi anapaswa kuwa na hekima na kuongoza watu wake kwa umoja wakati wa changamoto.
- Umoja na mshikamano hutusaidia kushinda vipindi vigumu vya maisha.

Novela

3. (a) Kuonyesha kuwa elimu na bidii ndizo silaha kuu za kujikwamua kutoka kwenye umaskini na kuleta matumaini mapya maishani.

(b)

- Mandhari ya mahali: Kijiji cha Kanyama, nyumbani kwa Mzee Juma, Chumbani kwa Amina, mashambani.
- Mandhari ya hali: Umaskini, dhiki, furaha
- Mandhari ya wakati: Ndani ya muda mfupi, dakika chache baadaye, kila siku.

(c)

- Mwenye kuwajibika/ Mtiifu: Anamsaidia Mzee Juma na mama yake kazi za shambani kabla ya kusoma.
- Mvumilivu/ Mstahimilivu: Hakukata tamaa hata aliposoma akiwa na njaa, uchovu au chini ya mwanga hafifu wa kibatari.
- Mwerevu/ Mwenye akili nyepesi: Alifaulu kwa alama za juu sana na kuwa mwanafunzi bora eneo zima.

(d) **Mbinu mbili za lugha zilizotumika:**

- Tashbihi: "...furaha ililipuka kama radi."
- Tashihisi/Uhaishaji: "Mvua iliponuna..."
- Jazanda/Istiara: "...ndani ya giza hilo, kulikuwa na mwanga mdogo..." (Giza kuwakilisha umaskini, mwanga kuwakilisha elimu).

- (e) Amina anaishi kwenye umaskini na dhiki katika Kijiji cha Kanyama lakini anasoma kwa bidii usiku kwa mwanga hafifu wa kibatari. Anafanya mtihani wa mwisho na kupita kwa alama za juu sana na kijiji kinasherehekea. Serikali ya kaunti inaguswa na kumpa udhamini wa karo ya masomo ya juu.

Tamthilia

4. (a)

- Maelekezo ya jukwaani (mabano/herufi za mlazo): Maelezo yanayoongoza matendo na hisia za wahusika.
- Migawanyo ya kimuundo: Matumizi ya sehemu (Sehemu ya 3) na onyesho (Onyesho la 2).
- Majina ya wahusika kuandikwa pambizoni kabla ya usemi wao.

(b)

- Elimu: Umuhimu wa kusoma kwa bidii kama ufunguo wa maisha.
- Nidhamu na maadili: Bibi na Sauti ya Babu wanasisitiza nidhamu na heshima kwa wazee.
- Ushirikiano/ Mshikamano wa kijamii: Kufanya kazi pamoja shuleni na kijijini (kama kulima na kujenga).
- Uwajibikaji: Umuhimu wa kijana kutumia anachonacho kwa manufaa ya jamii yake.

(c)

- Kueleza vitendo na mienendo ya wahusika jukwaani (kwa mfano: *Karima anaingia akiwa na begi, anachukua simu*).
- Kuonyesha hisia na toni za wahusika (kwa mfano: *akiwa na furaha, kwa mshangao kidogo, akitabasamu kwa huzuni*).
- Kuongoza mabadiliko ya jukwaa na taa (kwa mfano: *taa zinazima. Giza.*)

(d)

- Methali/ Semi: "Nidhamu ndiyo ufunguo wa mafanikio."
- Kuhamisha ndimi: "Discipline is the key to success."
- Istiara: "Elimu... ni mwanga wa maisha"/ "Teknolojia ni chombo, sio bwana."
- Utohozi: Teknolojia

Ushairi

5. (a) Shairi linaeleza maafa, hasara na mateso yanayosababishwa na janga la mafuriko kama vile kubomoka kwa nyumba, kuzama kwa mifugo na kilimo na kutoa wito wa usaidizi kutoka kwa Mungu na serikali ili kurejesha amani na kuboresha maisha.

(b)

- Serikali
- Wataalamu

(c)

- Tashihisi/Uhaishaji: "Mito hufoka ghafla..." (Mito imepewa sifa ya kufoka kama mwanadamu).
- Nidaa: "Ewe Mungu mlinzi!..." (Sauti ya kilio/wito).
- Takriri: Kurudiwa kwa neno "tele", "kimezama/ imezama".